HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI PROF. MARK MWANDOSYA (MP), KWENYE MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA, TANGA TAREHE 12 MACHI 2009

Mhe. Mohamed Abdulaziz (Mb), Mkuu wa Mkoa wa Tanga,

Ndugu Wilson Mukama, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji;

Mhe. Salim Kisauji, Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga;

Mhe. Bakari Mwapachu, Mbunge wa Tanga;

Mhandisi Raymond Mhando, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga;

Mhandisi Elizabeth Kingu, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maji Kibiashara, Wizara ya Maji na Umwagiliaji;

Ndugu Haruna Masebu, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA);

Ndugu Wenyeviti wa Bodi za Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Arusha Moshi, Morogoro;

Wakurugenzi wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga,

Mhandisi Archard Mutalemwa, Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Maji safi na Majitaka Dar es Salaam;

Mhandisi Alex Kaaya, Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maji safi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO);

Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Arusha, Moshi na Morogoro;

Ndugu Wanahabari kutoka vyombo mbalimbali;

Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga;

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

1. Utangulizi

Shukrani zetu nyingi ni kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuifikia siku ya leo. Kwa niaba ya Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji, na kwa niaba yangu mwenyewe, nachukua fursa hii kuwashukuru wote mlioitikia wito wa kuja kushiriki katika hafla hii muhimu, na ya kihistoria katika Sekta ya Maji hapa nchini, ya kuadhimisha miaka kumi tangu Mamlaka za maji zilipoanzishwa. Napenda kuwashukuru

kwa kunialika kuwa Mwenyeji Rasmi katika shughuli ya leo. Mmeacha kazi nyingine nyingi katika ujenzi wa Taifa. Hii inadhihirisha kuwa mnatambua umuhimu wa huduma ya Majisafi na uondoaji wa Majitaka katika miji yetu na katika Jiji hili la Tanga.

Kwa leo mtaniwia radhi. Nitatumia muda wenu tukumbushane tulikotoka na tulipo, ili tuwe na uelewa wa pamoja kuhusu tunakokwenda, na tunakwenda vipi, katika azma yetu ya kumpatia mwananchi ambaye ni mkazi wa mjini, maji safi, salama na ya uhakika.

2. Historia Fupi ya Mamlaka za Maji Mijini

NduguWageni Waalikwa, Chimbuko la kuanzishwa kwa Mamlaka za Maji nchini ni utafiti ambao ulifanywa na Wataalam wa Wizara yenye dhamana ya maji, mwaka 1992, wa kuona namna bora zaidi ya kutoa huduma kwa wananchi waishio mijini. Mwaka 1992 ni wenye kumbukumbu kwangu. Kwani nilikuwa Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Sikujua tulikuwa tunapanda mbegu itakayozaa matunda. Utafiti huo ulipendekeza kuanzishwa kwa vyombo ambavyo vingeweza kujitegemea na ambavyo vingekuwa karibu na wananchi, chini ya usimamizi wa Bodi zake. Kufuatia utafiti huo, utaratibu mpya wa majaribio wa kuendesha huduma za maji mijini ulianza mwaka 1994 kwa kutumia akaunti maalum chini ya Sheria ya Fedha (*Exchequer and Audit Ordinance*) ya mwaka 1961. Majaribio ya utekelezaji wa mfumo huo mpya yalianza kwa miji ya Arusha, Moshi na Tanga. Kutokana na mafanikio ya majaribio yale, mwaka 1997 Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Maji *(Waterworks Ordinance Cap 281*) ya mwaka 1956. Marekebisho hayo yalimpa madaraka Waziri mwenye dhamana ya maji mamlaka ya kuunda vyombo vinavyojitegemea, ambavyo vinajulikana kwa jina maarufu la Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini {*Urban Water Supply and Sewerage Authorities}* (**UWSA**). Kufuatia marekebisho hayo, mamlaka za majisafi na majitaka katika miji yote mikuu ya mikoa, isipokuwa Dar-es-salaam na Kibaha, zilianzishwa rasmi tarehe 1 Januari, 1998. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya mji wa Babati ilianzishwa mwaka 2003.

Kwa upande wa Dar-es-salaam na Kibaha, katika marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Taifa ya Maji Mjini - *{National Urban Water Authority}* (NUWA) yaliyofanyika mwaka 1997, uendeshaji wa huduma uliwekwa chini ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar-es-Salaam (DAWASA).

Katika kipindi cha nyuma huduma hizi zilikuwa zikizorota mwaka hadi mwaka kutokana na:-

- Ongezeko la watu.
- Kupanuka kwa makazi kusikoendana na ukarabati na upanuzi wa mitandao ya maji.
- Uchakavu wa miundombinu na mabomba ambayo mengi yalifungwa kabla ya Uhuru na hivyo, kusababisha uvujaji mkubwa wa maji.
- Huduma duni za uendeshaji na matengenezo.
- Uwekezaji mdogo katika sekta.

Lengo kuu la kuanzisha Mamlaka hizi, ni kuimarisha utoaji huduma za majisafi na uondoaji majitaka, kwa kujiendesha ili huduma ziwe endelevu. Nachukua fursa hii kuzipongeza kwa dhati kabisa, Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Tanga, Moshi na Arusha kwa kufanikisha majaribio ambayo yamewezesha kuanzishwa kwa Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika miji mikuu yote ya mikoa.

Mpaka sasa tuna jumla ya Mamlaka 19, kati ya hizo Mamlaka 11 (Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora na Tanga) zipo Daraja 'A'. Daraja hilo linahusu Mamlaka ambazo zinajitegemea katika gharama zote za uendeshaji na matengenezo, zikiwemo mishahara ya watumishi, gharama za umeme, na sehemu ya uwekezaji. Katika Daraja 'B', zipo Mamlaka 6 (Bukoba, Kigoma, Musoma, Singida, Songea na Sumbawanga) ambazo bado zinapata ruzuku ya kulipia sehemu ya gharama za umeme. Mamlaka zilizo kwenye Daraja 'C' ngazi ya mikoa ni mbili ambazo ni Babati na Lindi na katika ngazi za Wilaya na Miji midogo zipo mamlaka 106. Mamlaka zote za Daraja C bado zinapata ruzuku ya Serikali ya kulipa mishahara ya wafanyakazi wake pamoja na kulipia gharama za umeme na uwekezaji. Kwa mamlaka niliyopewa kisheia nimeidhinisha kupanda kwa miji ya Musoma na Songea kutoka daraja B kwenda A.

3. Sera, Mkakati, Usimamizi na Udhibiti

Sera ya Maji ya mwaka 2002, pamoja na mambo mengine, ina madhumuni ya kuwezesha uendelezaji na usimamizi endelevu wa utoaji huduma ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wakazi wa mijini. Madhumuni hayo yatafikiwa kwa kuweka malengo na kutoa miongozo na vigezo vya utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Mamlaka hizi na watekelezaji wengine. Nia ni kuboresha huduma. Sera inalenga katika masuala yafuatayo:

i) Kutoa mwongozo wa namna ya kuendeleza na kusimamia huduma ya majisafi na majitaka mijini kwa ufanisi.
ii) Kuweka mazingira mazuri yatakayoivutia sekta binafsi kuwekeza katika kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini.
iii) Kuhakikisha kuwa upo muundo mzuri wa kitaasisi unaovipa vyombo vya uendeshaji huduma ya majisafi na majitaka mijini madaraka ya kujiendesha kibiashara.
iv) Kuwa na mfumo madhubuti na wenye ufanisi katika ukusanyaji maduhuli yatokanayo na mauzo ya majisafi na uondoaji wa majitaka na hivyo kuongeza mapato na;
v) Kupunguza upotevu wa maji na kuboresha uondoaji wa majitaka.

Ndugu Waalikwa, maendeleo ya Sekta ya maji kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, yanazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Dira ya Taifa ya Maendeleo inalenga katika kuwapatia wananchi wote waishio vijijini na mijini huduma ya majisafi na salama ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa Dira hiyo umegawanywa katika malengo ya muda mfupi na muda

wa kati. Katika muda wa kati, Serikali imedhamiria kutekeleza Malengo ya Kimataifa ya Milenia, hususan lengo namba 7 ambalo kwa sekta ya maji ni kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu wasio na huduma ya majisafi na salama na huduma ya usafi wa mazingira, na kuweka mfumo shirikishi wa usimamizi wa rasilimali za maji ifikapo mwaka 2015.

Kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunafikia malengo ya Milenia, Serikali iliandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao utekelezaji wake ni wa miaka mitano, mwaka 2005 hadi 2010. Katika mkakati huo, Sekta ya maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi majisafi na salama, karibu na makazi yao, kwa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma hiyo vijijini kutoka **asilimia 53.5** mwaka 2004/2005 hadi **asilimia 65** na kutoka **asilimia 74** mwaka 2004/2005 hadi **asilimia 90** ya wananchi waishio mijini, ifikapo mwaka 2010.

Katika kuhakikisha kwamba malengo hayo yanafikiwa, mwezi Desemba 2006, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Washirika wa Maendeleo wamekubali kuchangia gharama za utekelezaji. Programu hiyo iliyoanza kutekelezwa rasmi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 imegawanyika katika programu nne ambazo ni: uboreshaji usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini; utoaji wa majisafi na uondoaji wa majitaka mijini; na uimarishaji wa taasisi za maji na kuzijengea uwezo.

Kuhusu utekelezaji wa programu ya maji safi na majitaka mjini, baada ya kuanzishwa Mamlaka za Maji Mijini, na usimamizi wake kuwa chini ya Bodi za Wakurugenzi, kazi kubwa ya Wizara imekuwa ni kuziimarisha na kuziratibu shughuli zake kupitia taarifa mbalimbali. Wataalam wa Wizara hushirikiana na uongozi wa Mamlaka katika kuhakiki hali halisi ya utendaji kwenye mamlaka husika. Uhakiki huu wa utendaji pamoja na Mikataba ya Makubaliano (MoU) kati ya kila Mamlaka na Wizara imezisaidia sana Mamlaka kuhakikisha kwamba vigezo vilivyowekwa na kukubaliwa kwa pamoja vinatekelezwa kwa ufanisi unaostahili.

Ndugu Wageni Waalikwa, katika kuhakikisha kwamba huduma zinasimamiwa na kudhibitiwa kwa mujibu wa sheria, Serikali imeunda Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *{Energy and water Utilities Regulatory Authority}* (EWURA) kupitia Sheria Na. 11 ya mwaka 2001, na marekebisho yake ya mwaka 2002, Kifungu Na. 414. Kazi kubwa ya EWURA ni kusimamia haki za mwananchi anayepata huduma na haki za mtoa huduma. Kuanzishwa kwa EWURA ilikuwa ni moja ya mikakati ya Serikali ya kurekebisha mfumo wa utawala na utendaji wa Serikali na Mashirika yake ili kuimarisha dhana ya Utawala Bora, na kuondokana na ukiritimba ambao ulikuwa ukidumaza uchumi wa nchi. Ili kuwa na mfumo wa ushindani wa kibiashara na soko huria utaratibu wa kuhakiki mizania *(checks and balances)* unahitajika ili kulinda maslahi ya wadau wote katika biashara huria, mtoa huduma kwa upande mmoja na mtumiaji wa huduma kwa upande wa pili. Kazi kubwa ya EWURA ni kuhakikisha kuwa mizania hiyo inakuwepo. Tangu kuanzishwa kwake, wateja wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA wamepewa fursa ya kutoa maoni kwa njia ya uwazi zaidi hususan, wakati wa kupandisha bei za maji

kwa lengo la kuboresha huduma husika na kuleta ufanisi zaidi katika Mamlaka zetu za maji nchini.

Vile vile kupitia Sheria ya EWURA, Baraza la Watumiaji Huduma za Maji na Nishati *(EWURA Consumer Consultative Council)* liliundwa mwaka 2005. Baraza hilo lina jukumu kubwa la kuwakilisha matakwa ya watumiaji huduma za maji, umeme, mafuta na gesi asilia na kutetea maslahi ya jinsia zote na wale ambao hawana uwezo. Baraza lina wajibu pia wa kushirikiana na vyombo vingine ambavyo tayari vimeundwa na vitakavyoundwa na kuimarishwa ili kupata uzoefu katika kujenga hoja na kuendesha mashauriano kwa misingi iliyo bora.

Ni wajibu wa baraza linatakiwa kufanya utafiti wa kisayansi na kiuchumi na kujenga hoja zenye nguvu ili kumtetea mtumiaji huduma pale inapobidi. Sheria ya Usimamizi wa Miundombinu-hodhi ya maji na nishati imelipatia Baraza majukumu mengi na ya msingi. Ni Wajibu wa Baraza kuwaelimisha wananchi ili walijue Baraza kwa lengo la kuwasilisha hoja zao kwake ili ziweze kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.

4. Kukua kwa Utoaji Huduma

Ndugu Waalikwa, sasa imepita miaka kumi (10) tangu Mamlaka za Maji Mijini zilipoanzishwa. Sisi sote ni mashahidi kwamba zimeboresha utoaji wa huduma. Naomba nirejee mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika kipindi hiki:-

(i) Katika miji mikuu ya mikoa, idadi ya wakazi wanaopata huduma imeongezeka kufikia asilimia **80** kwa wastani wa masaa **17,** kwa siku ikilinganishwa na asilimia **65** mwaka 1998.

(ii) Mamlaka zimeweza kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo **250,213** hadi mita za ujazo **288,539.7** kwa siku.

(iii) Kwa upande wa majitaka, kumekuwa na ongezeko la wakazi waliounganishwa kwenye mfumo wa majitaka kutoka wastani wa asilimia **2** na kufikia wastani wa asilimia **17**.

(iv) Makusanyo ya maduhuli pia yameongezeka kutoka shilingi bilioni **4.3** mwaka 1998 hadi shilingi bilioni **28** kufikia Juni 2008. Ongezeko hili limeziwezesha Mamlaka nyingi kutoa huduma nzuri pamoja na kuboresha na kuongeza mitandao ya majisafi kwenye maeneo yaliyokuwa hayana huduma.

(v) Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa maji imeongezeka kutoka **55,000** mwaka 1998 hadi kufikia wateja **210,970** mwaka 2008, sawa na asilimia **84** ya wateja wote kwenye miji ya makao makuu ya mikoa waliofungiwa dira za maji. Ongezeko hili limewezesha kupunguza upotevu wa maji **{***Uccounted For Water***}** - (UFW) kutoka asilimia **70** mwaka 1998 hadi asilimia **36** mwaka 2008.

(vi) Zaidi ya asilimia **90** ya Mamlaka zinatoa ankara sahihi za matumizi ya maji kwa wateja na kwa wakati, kutokana na matumizi ya komputa.

(vii) Mamlaka hizi sasa zinasambaza maji yenye ubora unaokubalika kutokana na kuwa na uwezo wa kugharamia madawa ya kusafisha na kuuwa vijidudu kwenye maji. Mamlaka za daraja A zipo katika mchakato wa kupata cheti cha ubora wa huduma ya maji katika kiwango cha kimataifa **(***International Standards Organization* - ISO). Hadi sasa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Tanga ndiyo pekee iliyopata cheti hicho, ilichokipata mwaka 2007. Naipongeza Mamlaka ya Tanga kwa kupata cheti hicho. Mamlaka hii imekuwa dira kwa Mamlaka zote nchini na imekuwa kati ya Mamlaka chache sana katika bara la Afrika kufikia kiwango hicho. Hatua hii ni muhimu kwani inalenga katika kumjali mteja na kuboresha huduma mara kwa mara.

(viii) Hali ya watumishi kwa ujumla imekuwa nzuri na tija imeongezeka kutokana na Mamlaka za daraja 'A' na 'B' kupanga na kuwalipa watumishi mishahara kutokana na makusanyo yao. Kuhusu watumishi wa Mamlaka za Daraja 'B' na 'C', hali zao pia zimeboreshwa kutokana na Bodi husika kupanga motisha mbalimbali kwa watumishi wao kutegemeana na makusanyo na kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

(ix) Kutokana na mwamko mkubwa na uhamasishaji uliopo kwa wananchi kuwa huduma ya maji ni ya kulipia, madeni ya Taasisi za Serikali yamepungua kutoka shilingi bilioni 2.2 mwaka 1998 hadi shilingi bilioni 1.4 mwakai 2008.

(x) Mamlaka zote zinafanyiwa ukaguzi wa hesabu (*Audited Accounts*) na Mkakaguzi Mkuu wa Serikali **(***Controller and Auditor General* - CAG) kwa wakati na kupata cheti cha usahihi **(***Certificate of Correctiness* - CoC). Mwaka 2006/2007 Mamlaka zote katika ngazi ya mkoa, isipokuwa Mtwara, Singida, Babati, DAWASA na DAWASCO zilipata vyeti safi *(Unqualified)*.

(xi) Miundo mbinu ya majitaka imeboreshwa katika miji ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa hivyo, kuondoa kero iliyokuwepo hapo awali ya majitaka kutiririka ovyo katikati ya miji. Kupitia Programu ya Maendeleo ya sekta ya Maji *{Water Sector Development Programme}* (WSDP) ujenzi na ukarabati unaendelea katika miji yote. Mradi mkubwa wa Kutoa Maji Ziwa Victoria na kupeleka Kahama na Shinyanga upo kwenye hatua za mwisho za majaribio, Mamlaka ya kusimamia uendeshaji wake chini ya Bodi nayo tayari imeundwa. Utakapokamilika, mradi huu utaligharimu Taifa zaidi ya shilingi bilioni 250. Fedha hizi zimetolewa na bajeti ya Serikali!

5. Maji safi na Majitaka Tanga

Ndugu Waalikwa, kwa kuwa tupo Tanga, naomba mniruhusu niseme machache kuhusu Mamlaka ya Maji safi na Majita Tanga. Mamlaka hii imeendelea kukua tangu ianzishwe. Sasa imekuwa miongoni mwa Mamlaka bora na mfano wa kuigwa hapa nchini. Mafanikio haya yamechangiwa kwa kasi kubwa na wadau wengi wakiwemo wafadhili mbalimbali, Serikali, Bodi na wafanyakazi na wakazi wa Jiji la Tanga wananchi waishio

kwenye bonde la mto Sigi. Wameelewa umuhimu wa maji katika maisha na hulipia huduma wanazopata kutoka Mamlaka. Mafanikio yaliyopatikana kwa Mamlaka ya Tanga ni pamoja na:-

(i) Kuongeza idadi ya watu wanaopata maji kutoka asilimia 80 kwa saa 20 kwa siku katika miaka kumi iliyopita, hadi kufikia asilimia 99 ya wakazi wote waishio kwenye eneo la katikati ya Jiji ambao hupata maji saa 24 kwa siku.

(ii) Kuongezeka kwa utoaji wa huduma ya majisafi katika eneo la pembezoni mwa Jiji kutoka asilimia 40 hadi kufikia asilimia 72 ya wakazi wa maeneo hayo katika kipindi cha miaka kumi.

(iii) Kupunguza maji yanayopotea kutoa asilimia 41.5 miaka kumi iliyopita, hadi kufikia asilimia 27.2.

(iv) Mmeongeza ufanisi wa kukusanya maduhuli kutoka asilimia 77 miaka kumi iliyopita, hadi kufikia asilimia 95.7.

(v) Utoaji wa huduma ya maji bure kwa kaya 94 za wasiojiweza ndani ya Jiji la Tanga.

(vi) Kupata cheti cha kimataifa cha **"***International Standards Organization* - (ISO)*"* 9001:2000 kinacholenga kutathimini utendaji mara kwa mara ili kuboresha huduma kwa wateja.

7. Maji na Mazingira

Ndugu Wananchi, mafanikio yote niliyobaini yanaweza yakawa endelevu iwapo tutatunza mazingira na vyanzo vya Maji. Mazingira yakiharibika maji hupotea. Maji yakipotea, mazingira huharibika zaidi. Ili maji yaendelee kupatikana Tanga, tuna wajibu wa kutunza mazingira ya bonde la mto Sigi. Changamoto kubwa ni kushughulikia tatizo la wachimbaji wadogo wa madini wanaovamia bonde la mto huo mara kwa mara.

Nawapongeza wananchi wa Mabuyani na Pande kwa kujitolea kulinda na kuhifadhi chanzo cha maji na miundombinu yake kupitia kamati shirikishi ya mazingira yenye uwakilishi kutoka sehemu mbalimbali za mto Sigi. Kwa kuthamini mchango wao, leo, kwa niaba ya Mamlaka, nitakabidhi darasa kwa shule ya Sekondari ya Pande. Naipongeza Mamlaka kwa kujali jamii inayowazunguka kwa kutoa misaada ya maendeleo.

Kuhusu usafi wa mazingira nina taarifa kwamba ni asilimia 16 tu ya wakazi wa Jiji la Tanga wameunganishwa katika mfumo wa majitaka. Waliobaki, hutumia vyoo vya mashimo na wengine hutumia makaro *(septic tanks)*. Kiwango hiki cha mfumo wa majitaka ni cha chini sana na hii inachangia katika ongezeko la magonjwa na uharibifu wa mazingira, hasa kwa wananchi wanaotumia vyoo katika maeneo yenye ardhi oevu. Changamoto ya Bodi ni kusimamia utekelezaji wa upanuzi wa mfumo wa majitaka Jijini

Tanga, na kuhusika na juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara yangu na Halmashauri ya jiji katika kuboresha usafi wa mazingira na maliwato.

8. Changamoto

Ndugu Waalikwa, Pamoja na jitihada zinazofanywa na Mamlaka za maji safi na majitaka, Mamlaka bado zina kazi kubwa katika kufikia malengo ya kitaifa niliyoyataja hapo awali. Hivyo basi natoa kwenu changamoto zifuatazo:

Uharibifu wa Vyanzo vya Maji
Kwa Mamlaka ya Tanga, uharibifu wa mazingira katika bonde la mto Sigi hutokana na shughuli zisizo endelevu. Bonde la mto Sigi ndiyo chanzo pekee cha maji kwa wakazi wa Jiji la Tanga. Natoa wito kwa Bodi kwa kushirikiana kwa karibu zaidi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupata suluhisho la kudumu la tatizo hili. Utekelezaji wa mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji utasaidia sana katika kukabiliana na changamoto hii na nyingine. Ni jukumu la Mamlaka zote kuhusika na ulinzi na hifadhi ya mazingira na vyanzo vya maji

Kuchelewa k ulipia Ankara za Majisafi na Majitaka
Kuchelewa kulipia ankara za majisafi na majitaka kutoka makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za Serikali ni tatizo katika Mamlaka karibu zote za Maji hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Desemba 2008 zaidi ya shilingi bilioni 30 zilikuwa zinadaiwa na Mamlaka za Maji nchini ambapo, DAWASCO pekee inadai zaidi ya shilingi bilioni 23 kutoka kwa wateja wake. Mamlaka ya Tanga wanadai zaidi ya shilingi milioni 450.

Natoa wito kwa wale wote wenye madeni kujenga tabia ya kulipa ankara zao kwa wakati kuepuka bughudha na usumbufu wa kusitishiwa huduma. Vile vile Mamlaka za Maji zichukue hatua za kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya maduhuli yao kwa wakati kuepuka malimbikizo.

Wimbi la Wizi wa Vyuma Chakavu
Kumejitokeza na kushamiri kwa wimbi la wizi wa vyuma ikiwa ni pamoja na mita za maji, mifuniko ya mashimo ya majitaka, mabomba ya maji, viungio mbambali vya mabomba ya maji katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Haingii akilini kwamba mita mpya ya maji inaweza kuwa ni chuma chakavu! Uharibifu huu unarudisha nyuma juhudi za Serikali na Mamlaka za Maji za kuwapatia wananchi maji. Natoa wito wananchi wawe walinzi wa miundombinu hii. Vile vile Mamlaka zishirikiane na uongozi wa Mikoa katika kuweka nguvu za pamoja ili kupambana na hujuma, uharibifu na uhalifu huu ambayo hakika ni yao.

Uvujaji/ upotevu wa maji (Unaccounted for Water-UfW)
Upotevu wa maji unakadiriwa kufikia wastani wa asilimia **36** kwa sasa ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kimataifa cha asilimia 20 au chini ya hapo. Mamlaka

zinatakiwa kuweka mikakati ya kuziba mianya yote ya upotevu wa maji ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa wakati.

Gharama kubwa za uendeshaji
Gharama kubwa za uendeshaji wa Mamlaka za majisafi na majitaka mijini bado ni tatizo kubwa. Mamlaka zinashauriwa kupunguza gharama zisizo za lazima kama zinavyotakiwa katika makubaliano na Wizara yangu.

Kufikia Malengo
Ili kuyafikia malengo ya MKUKUTA ya kuwapatia maji wakazi wa mijini kwa asilimia **90** ifikapo 2010, Malengo ya Milenia ya asilimia **95** ifikapo 2015 na asilimia **100** malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (NDV) ifikapo mwaka 2025, Mamlaka zote zinatakiwa zifanye kazi ya ziada, kwa kujituma na kuongeza tija.

Huduma duni ya uondoaji wa Majitaka

Huduma ya uondoaji wa majitaka bado si ya kuridhisha kutokana na uwekezaji mdogo na mwamko mdogo wa wananchi katika kuunganishwa kwenye mitandao. Mamlaka zinatakiwa kujitangaza, kuweka mikakati ya ziada ili kuongeza idadi ya wanaounganishwa kwenye mtandao. Pale ambapo miundombinu haipo, Mamlaka zitumie fursa ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ili kutafiti na hatimaye kujenga miundombinu hiyo. Mamlaka zihusike vilevile katika utekelezaji wa mkakati wa usafi wa mazingira mjini.

9. Shukrani

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote waliochangia katika mafanikio ya Mamlaka za Maji hapa nchini. Miongoni mwao ni Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la **KfW** ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika uwekezaji kwa kuboresha mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji maji katika Jiji la Tanga; Benki ya Dunia - **WB** kwa kugharamia upanuzi na ukarabati wa mifumo ya majisafi na majitaka sehemu mbalimbali hapa nchini mwaka 1998/1999; **DANIDA** kupitia Mpango Endelevu wa Miji mbalimbali hapa nchini mwaka 2002/2003 hadi 2006/2007, ambao kwa Jiji la Tanga walichangia katika kuendeleza mtandao wa majisafi wa urefu wa kilometa **65,** hasa katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji.

Washiriki wengine waliochangia kwenye mafanikio ya Mamlaka za Majisafi na Majitaka hapa Nchini ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika - **ADB**, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika - **BADEA**, Jumuiya ya nchi za Ulaya - **ACP-EU**, Shirika la Maendeleo la Norway - **NDF.** Wengine ni **Shirika** la Maendeleo la Ufaransa - **AFD,** Shirika la Maendeleo la ya kiufundi la Ujerumani - **GTZ,** Shirika la Msaada la Uswisi - **SECO,** Shirika la Ufundi la Ubelgiji - **BTC,** Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan - **JICA,** Shirika la Milenia la Marekani - **MCC** na Shirika la Makazi Duniani - **UN-HABITAT**. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuziwezesha Mamlaka za Maji Mijini kufikia hatua ambayo mafanikio yake tunajivunia.

Ndugu Wageni Waalikwa, Wizara yangu katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA, Milenia na *'Vision 2025'* kwa sasa inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Programme -WSDP)*. Mpango huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka 2006 na utatekelezwa hadi mwaka 2025, na unachangiwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo kutoka nchi marafiki kwa kupitia Mfuko Maalum wa Maji *(Basket Fund)*. Mpango huu utatumia jumla ya Dola za Marekani milioni **951** katika kipindi cha 2006 hadi 2011 katika kuendeleza Sekta ya Maji Mijini. Kati ya fedha hizo, Jiji la Tanga limetengewa Jumla ya Dola milioni **3.3.** Programu hii itakapokamilika hali ya uendeshaji wa Mamlaka zetu nchini itaimarika na kuziweka katika hadhi na viwango vya kimataifa. Changamoto iliyo mbele yetu ni namna ya kujipanga na kutekeleza programu hii ya maji (WSDP) ili ilete matokeo yaliyokusudiwa. Nawashukuru tena Washirika wetu kwa kuchangia Mfuko Maalum wa Maji

Ndugu Waalikwa, Mafanikio ya Mamlaka za Maji nchini yametokana na juhudi za Serikali katika kuweka misingi na mazingira mazuri ya sheria na sera zinazotekelezeka kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Kutokana na mafanikio haya, idadi ya wahisani na misaada na mikopo katika Sekta ya Maji sasa imeongezeka kwa kiasi kikubwa, ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya Mamlaka hizi kubuniwa. Tunatambua pia kwamba watumiaji wa huduma zetu za maji safi na majitaka wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kulipia huduma wanazotumia na wanaendelea kutoa maoni mbalimbali katika kuboresha huduma.

10. Hitimisho

Ndugu Wenyeviti, **Ndugu Wageni Waalikwa**, Wizara inafahamu kwamba baadhi ya Mamlaka za Majisafi na Majitaka ikiwemo Mamlaka ya Tanga, zimepiga hatua kubwa katika ufanisi na utoaji huduma. **Sifa tulizowapa zisiwaingie kichwani mithili ya 'mgema'**. Mnatakiwa kuanzia sasa kufikiri na kutenda tofauti na mazoea ili kuhakikisha mnafanya kazi kwa tija zaidi na wateja wanapata huduma bora zaidi na kwa gharama nafuu zaidi. Ni rahisi kufika kileleni lakini kazi kubwa ni kuendelea kubakia hapo. Hii ni changamoto kwa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Maji safi na Majitaka Tanga.

Ndugu Waalikwa, mwisho nawashukuru tena kwa mwaliko, na nawashukuru sana kwa usikivu wenu. Naomba tushirikiane kuendeleza Mamlaka za Maji nchini ili zifikie malengo ya Taifa katika Sekta ya Maji na azma ya Mamla zetu kujiendesha kwa kujitegemea. Namalizia kwa kuwatakia kila la heri Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga na Mamlaka nyingine nchini katika kuhakikisha tunatoa huduma bora, za uhakika na endelevu.

Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA